UN environment programme

# Barua kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji

## UNEP katika mwaka wa 2020



**Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) ni mhamasishaji mkuu wa masuala ya sayari na afya ya wanadamu. Kwa karibu miaka 50, UNEP imetumia sayansi ya kusaidia ulimwengu kuelewa madhara ya uzalishaji wa gesi ya ukaa unaofanywa na wanadamu wakati wa kufanya maendeleo yanayomaliza rasilimali kwa sayari, afya ya wanadamu na uchumi, na inaunga mkono sera na hatua za kusitisha na kukabiliana madhara haya.**

Lakini katika mwaka wa 2020, sayari ilijitetea. Janga la COVID-19 lilisababisha madhara makubwa, lilisababisha vifo na kudhihirisha kwa kiasi kikubwa zaidi ukosefu wa usawa. Uchumi unazorota kwa kina kikubwa sana. Kwa mara ya kwanza katika miaka 30, umaskini unaongezeka huku janga likisababisha ulimwengu kutoweza kutimiza ahadi zake za Ajenda ya 2030.

Kama majanga mengine yaliyotangulia, janga hili linahusiana na jinsi binadamu anavyoshughulika na mazingira kama kiini cha ukuzi wa uchumi. Mambo makuu yaliyowezesha kutokea kwa janga hili – hususa matumizi ya bidhaa na uzalishaji usio endelevu – ndio mambo yaleyale yanayoendeleza matatizo matatu makuu ya sayari: janga la tabianchi, janga la bayoanwai na mazingira na janga la uchafuzi na taka. Joto lilizidi kuongezeka ulimwenguni katika mwaka wa 2020, jambo lililochangia visa vya moto wa asili, ukame, mafuriko na uvamizi wa makundi ya nzinge waharibifu. Uharibifu kwa mazingira kwa ukulima, miundo msingi na makazi ya binadamu unazidi kuongezeka. Uchafuzi wa hewa, ardhi na bahari bado unasababisha vifo na kuharibu mifumo muhimu ya ekolojia.

Mwezi wa Desemba mwaka wa 2020, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa António Guterres aliyapa mambo haya kipao mbele kwenye ajenda. Alisema kwamba ni lazima binadamu wafanye amani na mazingira au wakabiliane na changamoto mbaya zaidi kuliko COVID-19 siku zijazo. Kufanya amani na mazingira kunahitaji kurudisha mfumo katika hali yake ya awali. Kunahitaji mabadiliko ya muda mrefu ya jinsi binadamu wanavyotoa na kutumia rasIlimali. Kunahitaji mabadiliko ya haraka na ya kudumu ili kuwa na ulimwengu unaofanya kazi na mazingira, si dhidi yake.

Katika mwaka wa 2020, licha ya usumbufu uliosababishwa na janga, UNEP ilijitahidi hata zaidi kushughulikia matatizo matatu makuu ya sayari, ikijumuisha kubadili mkondo wa baadhi ya kazi yetu ili kushughulikia madhara ya COVID-19 kwa mazingira, kama vile kuongezeka kwa uchafu na kuweka misingi ya kurejelea hali ya kawaida iliyo salama kwa mazingira baada ya janga. Pamoja na barua hii, ninawasilisha baadhi ya mambo makuu kutoka kwa kazi hii.

**Inger Andersen**
Anayefanya kazi Chini ya-Katibu Mkuu wa UN na
Mkurugenzi Mtendaji wa UNEP



# Mabadiliko ya Tabianchi

> “Tunakabiliwa na mambo matatu muhimu tunaposhughulikia tatizo la tabianchi: kwanza, tunahitaji kufikia kutozalisha gesi ya ukaa ulimwenguni pote ndani ya miongo mitatu ijayo. Pili, tunahitaji kuhakikisha kuwa ufadhili ulimwenguni kote unazingatia Mkataba wa Paris, unaoongoza ushughulikiaji wa mazingira ulimwenguni kote. Tatu, lazima tutumie mbinu inayozingatia hali ya maeneo mbalimbali ili kutunza ulimwengu.

**António Guterres,** Katibu-Mkuu wa Umoja wa Mataifa akizungumza tarehe 2 Desemba mwaka wa 2020 katika hotuba yake kuhusu Hali ya Sayari.



## Kupunguza uzalishaji wa gesi ya ukaa katika siku zijazo kupitia sayansi na majadiliano

Zaidi ya miaka mitano imepita tangu mataifa yalipojadiliana kuhusu Mkataba wa Paris wa kuzuia ongezeko la joto ulimwenguni katika karne hii lisizidi nyuzijoto 2 na kupunguza hadi nyuzijoto 1.5. UNEP kupitia Ripoti ya Emissions Gap ya kila mwaka, hufuatilia jinsi uwajibikaji unavyofikia lengo hili. Toleo la hivi karibuni zaidi, lililotolewa mnamo Desemba 2020, lilionyesha kwamba kudorora kwa uchumi kunakosababishwa na janga kutakuwa na athari ndogo kwa uzalishaji wa gesi chafu na hali ya joto. Kwa kutegemea Ahadi Zinazotolewa na Taifa (NDCs) ya hivi sasa, ulimwengu bado haufikii malengo ya Mkataba wa Paris. Wakati uohuo, Ripoti ya Production Gap, ambayo huchapishwa na UNEP pamoja na mashirika yanayoongoza na wanasayansi, ilibaini kwamba ulimwengu unahitaji kupunguza uzalishaji wa fueli za visikuku kwa asilimia 6 hivi kwa mwaka hadi mwaka wa 2030 ili kupata fursa ya kufikia lengo la nyuzijoto 1.5. Makadirio ya sasa yanadokeza ongezeko la kila mwaka la asilimia 2.

Ripoti hizi pia hutueleza jinsi ya kufikia malengo ya mazingira. Ripoti ya Emissions Gap ilibaini mipango ya kifedha ya kuimarisha uchumi baada ya janga kunaweza kusaidia ikiwa fedha zitaekezwa katika teknolojia zisizochafua mazingira, kutoa ruzuku kwa matumizi ya nishati jadidifu badala yakutumia nishati ya visukuku, na suluhisho linalotegemea mazingira. Uwekezaji kama huo unaweza kuweka ulimwengu katika angalau mkondo wa nyuzijoto 2 na kuunga mkono malengo mengine yanayohusiana na mazingira, jamii na uchumi.

Ili kuboresha uchumi bila kuchafua mazingira Ubia wa Hatua za Uchumi Usiochafua Mazingira, ambao UNEP hutoa sekritarieti,  uliweka mbinu ya kutoa msaada utakaowezesha kuboresha uchumi bila kuchafua mazingira katika nchi 20 zinazoshirikiana na UNEP. UNEP iliandaa ripoti kuhusu sheria, ikijumuisha iliyowaendea wanasheria wa Marekani kuhusu faida za kuboresha uchumi bila kuchafua mazingira, na ikawasilisha matokeo ya Ripoti ya Emissions Gap kwa Tume ya Ulaya.

Uchunguzi huu wa kisayansi katika Ripoti ya Emissions Gap ni muhimu sana katika mwaka huu, wakati ambapo Kongamano la Mabadiliko ya Tabianchi (COP26) lililocheleweshwa litafanyika. Kulingana na matokeo ya UNEP, ikiwa serikali mpya ya Marekani itatimiza ahadi zake za wakati wa uchaguzi za kujiunga na harakati zinazolenga kutozalisha gesi ya ukaa, nchi zinazosababisha zaidi ya asilimia 63 za uzalishaji wa gezi chafuzi  kabonidioksidi zitakuwa zimewajibika kwa kutochangia GHG. Lakini ahadi hizi lazima zifanywe kuwa sera na hatua thabiti za muda mfupi zijumuishwe katika NDCs thabiti kabla ya COP26. Kuhusiana na hili, UNEP inafanya kazi na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) ili kutoa msaada wa kiufundi kwa nchi zinazoandaa NDCs zao zilizoboreshwa.

> “
>
> Kama Wasimamizi wa COP26, tutatumia matokeo ya Ripoti hii ya [Emissions Gap] … na pia tutatumia Ripoti ya Adaptation Gap inayokuja ili kuendelea kuhamasisha dunia kujitolea zaidi kuhusiana na mambo yote ya msingi kwenye Mkataba wa Paris.
>
> **Archie Young**, Mtetezi Mkuu wa Tabianchi wa COP26, Uingereza na Kaskazini mwa Ireland

Hatua katika sekta ya majengo na ujenzi ni muhimu ili kuwe na NDCs thabiti na kuboresha uchumi bila kuchafua mazingira baada ya janga (ona Ripoti ya Hali ya Ulimwengu ya 2020 ya Majengo na Ujenzi). Miundo msingi endelevu inaweza kufanyiza tofauti kubwa kwa tabianchi, mazingira na uchafuzi wa mazingira –sababu iliyopelekea UNEP kushirikiana na wabia kuunda Njia nzuri na miongozo bora zaidi ya sekta hiyo. {Cool Coalition} inayoongozwa na UNEP hufanya kazi ili kuhakikisha faida kubwa za tabianchi kwa kuboresha kupoesha, na kuboresha matumizi ya nishati kwa njia pana.

## Miaka 35 ya Makubaliano ya Vienna

Mwaka uliopita ulikuwa maadhimisho ya 35th ya Makubaliano ya Vienna ya Utunzaji wa tabaka la Ozoni. Kupitia Makubaliano ya Mkataba wa Montreal, ni kana kwamba mataifa yameondoa vichafuzi vinavyoharibu ozoni, kumaanisha ozoni inayolinda sayari kutokana na miale hatari sasa inarekebishwa. Lakini Mkataba wa Montreal haujakamilishwa. Marekebisho ya Mkataba huu yaliyofanyiwa Kigali yanafanya mataifa yawajibike kupunguza hydrofluorocarbons zinazoongeza joto zinazotumika kupoesha. Badiliko hili, linalokadiriwa kuepuka ongezeko la joto la nyuzijoto 0.4 ulimwenguni kufikia mwaka wa 2100, lilikubaliwa na mataifa 21 zaidi katika mwaka wa 2020, hivyo kuleta jumla ya mataifa kufikia 112. UNEP husimamia Sekritarieti za Mfuko wa Kimataifa na Ozoni, na pia hutumika kama Mwekahazina, na ni Taasisi inayohakikisha Utekelezaji wa Mfuko wa Kimataifa.

Sehemu nyingine kuu ya sayansi na majadiliano ilikuja kwa njia ya Ripoti ya Magari Yaliyotumika na Mazingira, ambayo iliangazia maswala ya tabianchi na ubora wa hewa yanayotokana na nchi zilizostawi kuuza magari yasiyofaa na ambayo yametumika na yanayochafua hewa kwa nchi zinazostawi na ilihitaji viwango vya chini vya ubora vinavyokubalika. Kupitia msaada kutoka kwa UNEP na kwa uongozi wa Ghana, Kamisheni ya Kiuchumi ya nchi za Afrika Magharibi ilitangaza viwango dhabiti zaidi vya magari mwaka jana. Maagizo haya yanazuia kununua magari mepesi na yaliyo zaidi ya miaka tano na linalenga kuongeza maradufu utendakazi wa magari kufikia 2030. Sheria hizi ni hatua kubwa ya kupunguza uchafuzi wa gesi zinazoongeza joto ulimwenguni katika eneo ambalo ni nyumbani kwa zaidi ya watu milioni 400, na ambapo magari mengi yamezeeka.

## Husaidia watu walio na uwezo mkubwa wa kuathiriwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi

Jambo lingine la kupewa kipao mbele ni kusaidia nchi zinazostawi na jamii zinazoweza kuathirika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, ambazo zitaongozeka hata ikiwa ulimwengu utafikia malengo ya Mkataba wa Paris Ripoti ya Adaptation Gap na Hali ya 2020 ya UNEP inaonyesha bado ulimwengu hauchukulii kwa uzito ufadhili wa mabadiliko. Ufadhili bado uko chini sana wa viwango vinavyohitajiwa na hatua nyingi bado hazijapunguza hatari. Ulimwengu unahitaji kuwajibika katika kutimiza Mkataba wa Paris kuhusiana na ufadhili kutegemea na eneo.

UNEP pia inachukua hatua madhubuti za kusaidia nchi kushughulikia hali kutegemea na eneo. Mwaka wa 2020, UNEP ilisaidia mataifa zaidi ya 50 kuweka mikakati ya kitaifa ya kushughulikia hali kutegemea na eneo na mifumo ya kuonya mapema kuhusu mabadiliko ya tabianchi, na ilizindua miradi mipya nchini Benin, Ghana, Iraq, Lesotho na Mauritania. Kupitia kwa Global Environment Facility Blue Forests Project, UNEP ilisaidia uzinduzi wa miradi ya soko la gesi ya ukaa la mikoko nchini Kenya na Madagascar, ambayo inashughulikia kutunza na kuboresha kwa takribani hekatri 2,000 za mikoko na kuwezesha angalau watu 20,000 kuwa na kipato.

## Kubadili sekta za kibinafsi na za kifedha

Pia, ni lazima sekta ya kibinafsi ichukue jukumu la kuchukua hatua kuhusiana na tabianchi. Ushirikiano wa sekta ya umma na sekta ya kibinafsi unaanza kuimarika, huku UNEP ikichukua nafasi muhimu kupitia Mradi wa Kifedha na uwajibikaji mbalimbali.

Muungano wa mfuko wa AGRI3, ulianzishwa na UNEP na wabia wa benki, unalenga kukusanya dola bilioni 1 za Marekani kwa ajili ya ufadhili wa mazingira na ukulima unaojali mazingira na misitu. Shughuli za kwanza za hazina – kutunza misitu na uboreshaji wa mashamba ya malisho yaliyodorora huko Mato Grosso, Brazili, na ukulima endelevu wa pilipili katika eneo kubwa zaidi la Chongqing China – lilifungwa Desemba 2020, na mchango wa milioni 90 dola za marekani kutoka kwa serikali ya Uholanzi, Rabobank na Mfuko wa Kushughulikia Mazingira Duniani.

### Maendeleo ya haraka kupita gesi ya metheni

Metheni ni gesi yenye uwezo mkubwa zaidi wa kuongeza joto la tabianchi kuliko kabonidioksidi, ilihali inakaa kwenye hewa kwa muda mfupi zaidi. Ikisimamiwa na UNEP na kuongozwa na Muungano wa Mazingira na Hewa Safi, Tume ya Ulaya na Hazina ya Kulinda Mazingira, Ubia wa Mafuta na Gesi ya Metheni unajumuisha kampuni 62 zinazowakilisha asilimia 30 ya uzalishaji wa mafuta na gesi. Lengo ni kupunguza uzalishaji wa gesi chafu kwa asilimia 45 kufikia mwaka wa 2025 na asilimia 60-75 kufikia mwaka wa 2030. Katika mwaka wa 2020, ubia huo ulizindua mfumo mpya bora wa kuripoti ili kuboresha uwazi kuhusu uzalishaji wa gesi ya metheni kutoka kwa sekta ya metheni.

Washiriki wa Muungano wa Nchi Zilizoazimia Kuondoa Gesi Zinazoongeza Joto Ulimwenguni – mojawapo wa uwajibikaji dhabiti na majadiliano na wawekezaji na biashara zinazoendelezwa na Mradi wa Fedha – wamejitolea kupunguza uzalishaji wa gesi za ukaa kwa asilimia 16 hadi 29 kufikia mwaka wa 2025. Hii ni hatua kubwa ya kwanza kuelekea kuondoa gesi zinazoongeza joto ulimwenguni kufikia mwaka wa 2050. Wakiwakilisha mali inayosimamiwa ya dola trilioni 5.1 za Marekani, muungano huo utakuwa na athari kubwa kwa uzalishaji wa gesi chafu wakati ujao ulimwenguni.

Wakati uo huo, katika kuunga mkono juhudi za Katibu Mkuu za kuongeza ufadhili wa Ajenda ya 2030, UN-REDD na washirika wao walizindua jitihada zinazolenga kupunguza uzalishaji wa gesi chafu kila mwaka kwa tani bilioni moja – ambayo ni sawa na kuondoa asilimia 80 ya magari kwenye barabara za Marekani – kupitia kwa Shindano la Green Gigaton. Jumla ya gharama ya mradi huo ni kati ya dola za Marekani bilioni 10 na bilioni 15 kwa mwaka kufikia mwaka wa 2025.

> “ Napongeza juhudi za UNEP na miradi haswa zinazojihusisha na Kanuni za Uwajibikaji katika sekta ya Benki na Muungano wa Nchi Zilizoazimia Kuondoa Gesi Zinazoongeza Joto Ulimwenguni – ambazo kihalisi ni kufanya kanuni ziwe matendo.
>
> **Mark Carney,** UN Mjumbe Maalum wa Mabadiliko la Tabianchi na Fedha na Mshauri wa masuala ya kifedha wa UK wa COP26, na Gavana wa awali wa Benki ya Uingereza

# Mazingira na Bayoanuai

> Kufanya amani na mazingira ndiyo jukumu kuu la karne ya 21st. Lazima kupewe kipao mbele, na kila mtu, kila mahali.
>
> **António Guterres**
> Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa



## Kurudisha juhudi za kushughulikia bayoanuai duniani mahali pake

2020 ilipangiwa kuwa mwaka bora wa mazingira. Licha ya kwamba COVID-19 ilichelewesha hatua muhimu, kipau mbele kwa bayoanuai kuliongezeka kwa kiwango kikubwa. Mkutano Mkuu wa UN wa Bayoanuai wa kwanza kabisa kutokea na Ahadi ya Viongozi kwa Mazingira ulihimiza uwajibikaji wa kimataifa wa kukomesha na kukabiliana na uharibifu wa bayoanuai. Hili ni muhimu kwa sababu mazingira yako mashakani. Sekritarieti inayosimamiwa na UNEP iliandaa Kongamano la Viumbe Anuwai (CBD) na kutoa ripoti ya Global Biodiversity Outlook, katika mwaka wa 2020 iliyoonyesha kuwa, licha ya kusonga mbele, Malengo ya Bayoanuai ya Aichi hayajatimizwa. Kupitia Kituo cha UNEP cha Kufuatilia Uhifadhi Ulimwenguni (UNEP-WCMC), UNEP ilishikilia nafasi muhimu katika kuleta pamoja data ya utafiti huu, ikijumuisha kusasisha, kuthibitisha, au kuongeza rekodi za maeneo yaliyolindwa zaidi ya 200,000 na hatua zingine za uhifadhi zinazotegemea eneo katika Data Iliyolindwa ya Sayari.

Lengo muhimu katika mwaka wa 2021 ni ulimwengu kukubaliana kuhusu mfumo mpya wa bayoanuai kwenye mkutano wa 15th wa Kongamano la Vyama kwa CBD huko Kunming, China. Katika mwaka wote wa 2020, UNEP ilihamasisha kuhusu mikakati mikuu inayoweza kupimwa ambayo inategemeza maeneo ya uhifadhi makubwa zaidi, na yaliyosimamiwa vizuri zaidi, ukulima na ufugaji wa samaki unajali bayoanuai, ambao ndio mwisho wa ruzuku hatari, na kuacha uchimbaji madini wenye madhara na kushika mitindo ya matumizi na uzalishaji kwa njia endelevu. Licha ya janga la korona, Sekritarieti ya CBD aliendelea kuweka msingi kwa makubaliano hayo mapya muhimu, yanayoleta pamoja wataalamu kusasisha mikakati ya kutozalisha hewa chafu na, kwa ushirikiano na UNEP, kuchochea kuhusika kwa Makubaliano ya Kimataifa ya Mazingira katika mchakato huo.
.

> “
>
> Inaleta pamoja uthibitisho wa hali ya juu zaidi ya hali ya mazingira ulimwenguni kote na inapaswa kuthaminiwa.
>
> **Profesa Jane Memmott,** Rais, wa Jamii ya Kiekolojia ya Uingereza kuhusu Mtazamo Bayoanuai Duniani

## Kutunza na kuboresha mifumo ya ekolojia na bayoanuai

Ripoti ya UNEP kwa ushirikiano na na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo, Kuzuia janga linalofuata – Magonjwa yanayoambukizwa kutoka kwa wanyama na jinsi ya kuyayuia kuenea, ilionyesha kiini hasa cha magonjwa yanayoambukizwa kutoka kwa wanyama kama vile COVID-19 na iliangazia kwamba afya ya wanadamu, wanyama na sayari lazima ishughulikiwe kama swala moja wakati wa kuunda sera – jambo linalojulikana kama mbinu ya “One Health”. Kufuatia mbinu hii, UNEP ilianza kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula (FAO), Shirika la Afya Duniani na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani kama kikosi kimoja cha kusaidia kuzuia magonjwa yanayoambukizwa kutoka kwa wanyama.

Mwaka wa 2021 ni mwanzo wa Muongo wa UN wa Kuboresha Mfumo wa Ekolojia. Muongo huu – ukiongozwa na UNEP na FAO – unajizatiti kuzuia na kukabiliana na uharibifu na udororaji wa mifumo ya ekolojia ya nchi kavu na ya baharini. Suluhisho hili linalotegemea mazingira linaweza kutengeneza matrilioni ya madola katika huduma za mazingira kwa kuhifadhi bayoanuai, kuboresha mifumo ya ekolojia ya uzalishaji na kurudisha kiwango kikubwa cha gesi ya ukaa kwenye ardhi. Mwaka wa 2020, UNEP na wabia wake waliweka msingi wa muongo huu kwa kufanya mashauriano na umma ulimwenguni, kukamilisha na kutoa mikakati, na kutayarisha vifaa ili kuwezesha kufuatilia na kutekeleza kwa njia bora zaidi katika muongo huo.

UNEP ilifurahia kualikwa na FAO kushirikiana katika kuandika na kuzindua Ripoti ya Hali za Misitu Duniani, ambayo mwaka huu iliangazia masuluhisho bunifu ya kutunza bayoanuai ya msitu licha ya kudorora na kukatwa kwa misitu kwa viwango vinavyotisha. UNEP pia ilizindua Mtandao Mpya wa Kimataifa wa Mataalamu wa Nyasi za Baharini na kuchapisha ripoti ya kwanza ya kimataifa kuhusu umuhimu wa mifumo ya ekolojia ya nyasi za baharini kwa watu, bayoanuai na kwa mazingira – zinazochangia uzalishaji wa samaki, kuboresha maji na kulinda kingo za bahari. Mtandao huo unasaidia mradi wa kwanza ulimwenguni wa soko la gesi ya ukaa la nyasi ya baharini nchini Kenya.

UNEP pia ilichukua hatua zifaazo kuhifadhi wanyamapori. Nchini Nigeria na Zambia, msaada wa UNEP unawezesha askaripori kupunguza ujangili na biashara ya bidhaa zinazotoka kwa ndovu. Kwenye Hifadhi ya Wanyama ya Yankari nchini Nigeria, mojawapo ya maeneo kadhaa ya miradi, ni ndovu mmoja tu ndiye ameuawa kwa kipindi cha zaidi ya miaka tano. Kupitia kazi ya Kongamano la Kimataifa la Biashara la Spishi za Wanyama na Mimea Zilizo Hatarini (CITES) na UNEP-WCMC, rasilimali ziliwasilishwa mwaka huo ili kuwezesha maafisa wa forodhani na wengineo kutekeleza sheria ya CITES ya biashara za kimataifa za wanyamapori.

Pia, jambo lingine muhimu ni kongomano la 13 la nchi wanachama wa (COP13) kwa Kongamano la Viumbe Wanaohamahama, lililofanyika huko Gandhinagar, nchini India. COP13 lilikuwa kongamano kubwa zaidi katika historia, na liliongeza viumbe 10 vipya kwenye orodha yake.

## Kufadhili uhifadhi na uboreshaji

Ufadhili ni muhimu kwa kulinda, kuhifadhi na kusimamia mazingira kwa njia endelevu kama tu ilivyo na mabadiliko ya tabianchi. Hapa pia, UNEP ikifanya kazi na wabia, ina ufadhili mpya unaozidi kukua. Kwa ushirikiano na wabia, UNEP ilianzisha Restoration Seed Capital Facility iliyofadhiliwa na Ujerumani na Luxembourg kwa Yuro milioni 25. Hili linalenga kuchangisha kiwango cha chini cha dola milioni 170 ili kuwekeza kwa miradi ya kupanda misitu maeneo iliyokatwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Mfuko wa Kimataifa wa Miamba ya Matumbawe unalenga kuwekeza dola milioni 500 katika kipindi cha miaka kumi ijayo ili kuboresha afya ya matumbawe ambayo vinginevyo itatoweka kabisa ndani ya miaka 30. Mradi wa Fedha wa UNEP sasa una Mikakati Endelevu ya Kifedha ya Uchumi wa Maji, ambayo ni jukwaa jipya linaloleta pamoja taasisi za kifedha kufanya kazi pamoja na wanasayansi, mashirika makubwa na asasi za kiraia.



# Uchafuzi na takataka

Tatizo la uchafuzi wa hewa na takataka, kama matatizo ya tabianchi na mazingira, kwa kiwango kikubwa kinachochewa na matumizi na uzalishaji wa bidhaa usioweza kuendelezwa. Kama vile UNEP ilivyosimamia Jopo la Rasilimali za Kimataifa ripoti ya Biashara Endelevu ya Rasilimali inaonyesha, kila tani ya rasilimali zinazouzwa kati ya mataifa zinahitaji zaidi ya mara tatu ya malighafi kutoka kwa nchi inayouza. Zaidi ya thuluthi moja ya tani bilioni 92 ya rasilimali zilizotolewa katika mwaka wa 2017 zilitumika kuzalisha bidhaa za biashara. Kwa hiyo, kushughulikia uchafuzi wa mazingira na takataka kunahitaji hatua kuelekea mazoea ya matumizi na uzalishaji endelevu, ambayo pia ina faida kubwa kwa tabianchi na mazingira.





## Uchafuzi wa hewa

Uchafuzi wa hewa unachangia vifo vya mapema vya watu milioni saba kila mwaka, hasa katika nchi zinazostawi, ambayo inahusianishwa na ongezeko la uwezekano wa kuathiriwa vibaya na COVID-19. Ili kusaidia kujaza pengo la data kuhusiana na ubora wa hewa katika nchi zinazostawi, UNEP ilishirikiana na taasisi zingine ya UN na sekta ya kibinafsi kuzindua jukwaa kubwa zaidi ulimwenguni la data ya ubora wa hewa katika miji. Kifaa hiki kilichoenea katika miji zaidi ya 7,000, kinawezesha sera na bidhaa salama zaidi kwa mazingira, na kinawezesha wananchi kufanya viongozi wao wawajibike.

Mwaka uliopita, Kazakhstan ilifuatilia mapendekezo ya UNEP ya ubora wa hewa. Almaty, ambalo ni jiji kubwa zaidi katika nchi hiyo, ilianza kutumia sayansi ya wananchi kujaza data, na kuifanya ifike kwa umma. Senza 18 za Kupima ubora wa hewa sasa zimewekwa katika sehemu mbalimbali mjini Almaty, na zingine kwenye miji mingine mitano katika nchi hiyo. Wakati huohuo, jiji hilo linatafuta hatua za kuboresha hewa, pamoja na kufanya kituo cha uzalishaji wa umeme kwa kutumia mvuke kiwe cha kisasa zaidi.

Usafiri usiochafua mazingira ni muhimu kwa ubora wa hewa na UNEP inahusika katika miradi mingi ya kufanyiza usafiri wenye uchafuzi mdogo. Kando na kufanyia kazi viwango vya magari yaliyotumika, jukwaa la KUSONGA katika Amerika ya Latini na Karibian linasaidia kuepuka usafiri unaochafua mazingira, ikiwa ni pamoja na kusaidia nchi kufanyiza mikakati ya kitaifa ya usafiri wa umeme Mradi mwingine kwenye eneo la Asia-Pacific ni kusaidia nchi katika malengo yao ya kitaifa – kama vile Thailand, ambayo inalenga kuwa na magari ya umeme milioni 1.2 kwenye barabara zake kufikia 2036.

Kufuatia Azimio la Baraza Kuu la UN, UNEP iliwezesha kuwepo kwa maadhimisho ya kwanza ya Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi kwa anga za bluu, pamoja na Muungano wa TMazingira na Hewa Safi. Siku hiyo iliyozinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Korea, Moon Jae-inilihamasisha kuhusu masuluhisho kwa uchafuzi wa hewa.



## Kushughulikia uchafuzi wa bahari na tatizo la takataka

Makubaliano ya Basel yenye uanachama wa Wahusika 188, ya kudhibiti takataka hatari kati ya mipaka ni karibu yajumuishe ulimwengu wote, kumaanisha karibia nchi zote zinatarajiwa kuyafanyia marekebisho (yaliyoanza kufanya kazi mnamo Januari 1, 2021) yanadhibiti zaidi usafirishaji wa takataka za plastiki kati ya mipaka.

Huko Asia, mradi wa UNEP ulishiriki ujuzi wa kisayansi kuhusiana na uchafuzi wa plastiki katika mto Ganges, Mekong na mito mingine huko Asia. Kutokana na hali hiyo, Tume ya Mto Mekong na majimbo yake yanafanyiza mpango wa kusimamia na kufuatilia takataka ya plastiki kutoka kwenye bonde la mto Mekong kufikia mwaka wa 2022.

UNEP ikifanya kazi na Wakfu ya Ellen McArthur na Ahadi Mpya za Kimataifa Kuhusiana na Uchumi wa Plastiki Mpya wa UNEP walifuatilia maendeleo makubwa ya kampuni nyingi kubwa ya kutumia vitu vinavyoweza kutumika tena katika plastiki za kupakia na kuondoa vitu kama vile mifuko na mirinja ya plastiki inayotumika mara moja.

Kamati Maalum ya Ad Hoc Kikundi cha Wataalamu Kuhusiana na Uchafu wa Baharini na Plastiki Ndogondogo, iliyoanzishwa chini ya Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa ilikamilisha kazi yake katika mkutano wa nne uliofanywa mwezi wa Novemba mwaka wa 2020. Wengi katika kikundi hicho waliunga mkono makubaliano ya kimataifa yanayohusu takataka ya baharini, jambo linaloweza kuchangia hatua zaidi na kufungua ufadhili wa kushughulikia swala hili.



## Kupunguza madhara ya afya na mazingira kutokana na kemikali na majanga

Makubaliano ya Minamata, yaliyopata jina lake kutokana na jiji la Japani ambako watu walipata magonjwa ya kupooza baada ya kuathiriwa na sumu yenye zebaki iliyotokana na maji taka ya kampuni, ilipiga hatua kuu katika mwaka wa 2020 – tarehe ya mwisho ya waliotia sahihi kuacha kutengeneza, kuuza na kununua bidhaa zenye zibaki zilizoorodheshwa kwenye Makubaliano hayo. Vipima joto vyenye zebaki na bidhaa zingine zinabadilishwa na vifaa vingine mbadala, na nchi nyingi zimepiga marufuku bidhaa zenye zebaki za kufanya ngozi iwe nyeupe zaidi.

Janga la bwawa la Brumadinho nchini Brazil la mwaka wa 2019 lilikuwa kikumbusho kwamba viwango vya kimataifa vinahitajika kudhibiti mabwawa ya uchimbaji madini ili kampuni na watungaji wa sheria za kitaifa waweze kulinda jamii, wafanyakazi na mazingira. Kufuatia janga hilo, UNEP ilihusika katika Utathmini wa shughuli za uauzi duniani, ambao ulipelekea uzinduzi wa kanuni za uauzi viwandani duniani, zitakazoongoza shughuli zote za uauzi na uchimbaji madini.

Katika mwezi wa Agosti mwaka wa 2020, ndani ya saa 48 baada ya kiwango kikubwa cha ammonium nitrate kilichokuwa kimehifadhiwa katika bandari ya Beirut kilipolipuka, Kitengo cha Pamoja cha Mazingira cha UNEP-OCHA kilikuwa na watu kwenye eneo wakishauri viongozi, na kufanya kazi pamoja na timu kubwa zaidi ya UN ili kuwezesha Uchunguzi wa Haraka wa Madhara na Mahitaji uliochangia jitihadi za kurudia hali ya kawaida.



## Kushughulika na takataka ya COVID-19

UNEP inajizatiti kushughulikia ongezeko la takataka kutokana na janga. Kuhusiana na hili, UNEP ilitoa ushauri wa kiufundi kuhusu kushughulikia takakata ya kitiba kwa Afghanistan, Haita, Sudan Kusini na Sudan, pamoja na walinda amani wa UN. Zaidi ya hilo, UNEP ilichapisha miongozo ya kushughulikia takataka mango ya kitiba na manispaa, iliyofikia maelfu ya watu katika nchi zaidi ya 150.

Huko India, Afghanistan, Haiti, Sudan Kusini na Sudan, UNEP ilitoa kwa serikali ushauri unaofaa wa kushughulikia takataka. Huko Afrika Kusini, UNEP iliwezesha uchunguzi wa mahitaji ya COVID-19 ili kubaini mikakati ya kitaifa ya kurudia hali ya awali.

# Kutetea na kushirikiana kuleta mabadiliko

> Shughuli za binadamu ndiyo kiini cha matatizo yetu. Lakini hilo linamaanisha hatua ya binadamu inaweza kusaidia kuyatatua.

**António Guterres**
Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa



Kiwango cha mabadiliko yanayohitajika ili kushughulikia matatizo matatu ya sayari kinaweza tu kufikiwa ikiwa kila mmoja atahusika. Hiyo ndiyo sababu UNEP inajihusisha na kujenga ushirikiano katika sekta zote na kuchochea uajibikaji wa kibinafsi na hatua za kushughulikia mazingira – pamoja na kushirikiana na walimu, sekta za starehe na jamii za kidini.

Tarehe muhimu katika kalenda ya UNEP ni Juni 5, Siku ya Mazingira Duniani. Katika mwaka wa 2020 – licha ya janga la korona – Colombia, ikishirikiana na Ujerumani, ilisimamia sherehe za Siku ya Mazingira Duniani, zilizofanywa moja kwa moja mtandaoni kutoka Bogotá. Rais wa Kolombia Iván Duque Márquez aliongoza mwito kote ulimwenguni kwa kutangaza ni "Wakati #WaMazingira." Serikali, sekta ya kibinafsi, asasi za kijamii na mamilioni ya watu mmojammoja ulimwenguni pote – wengi wao wakiwa wamefungiwa manyumbani mwao – walijiunga katika matukio ili kutambua umuhimu wa mazingira kwa afya yetu, uchumi wetu na jamii zetu.

## Mitindo endelevu

Sekta ya mitindo inatumia lita trilioni 215 za maji na kinatoa tani bilioni 3.3 za gesi za ukaa duniani kila mwaka. Ili kudhibiti madhara ya mitindo ya haraka, ripoti ya UNEP inasaidia wazalishaji na wanunuzi wafanye maamuzi yaliyo salama zaidi kwa mazingira kwa kutambua madhara ya nguo kwa tabianchi, ardhi, mifumo ya ekolojia, maji, afya ya wanadamu na maswala ya kijamii. Wanamitindo kama vile Balozi wa Nia Njema Eneo wa UNEP Rami Kadi – ambaye mkusanyo wake wa majira ya mvua/kiangazi 2020 ulijumuisha nguo iliyotengenezwa kutoka kwa plastiki iliyotumika – wanatumia majukwaa yao kwa njia nzuri.

Katika mwaka wa 2020 kulikuwa na Shindano la Run Wild – programu ya rununu ambapo wakimbiaji wanalinganisha umbali halisi wa safari ya kakakuona, chui milia na ndovu waliowekewa kifaa cha GPS – ikipitisha lengo lake la wakimbiaji milioni moja.

UNEP ilishirikiana na TED kubuni Earth School – mradi mkubwa zaidi kuwahi kushuhudiwa wa kuelimisha kupitia mtandaoni. Jukwaa hili linaloelimisha, linalenga watoto na vijana kati ya umri wa miaka 5 na 18, lina shughuli 30 zinazoshughulikia mada kama vile takataka baharini, bayoanuai na mabadiliko ya tabianchi. UNEP pia ilishirikisha wachezaji kupitia Playing for the Planet Alliance. Ahadi kutoka kwa viwanda vya michezo ya video ni pamoja na usalama wa mazingira katika michezo, kupanda mamilioni ya miti na kupunguza matumizi ya plastiki – inayolingana na kupunguzwa kwa tani milioni 30 ya vichafuzi kufikia vya $CO_2$ kufikia 2030.

Kwa kushirikiana na serikali na mashirika ya kidini, UNEP iliandaa la kimataifa la dini mbalimbali lililokuwa na wawakilishi wa dini 12 kutoka kwa nchi 60 na kupelekea kuhidhia kwa matamko yanayotoa wito wa Muungano Mpya wa Dini wa Kushughulikia Mazingira, yatakayowasilishwa kwa kikao cha tano cha Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa la tano (UNEA-5).

# Kukumbatia Mabadiliko ya Kidijitali

COVID-19 ilionyesha uwezo wa teknolojia ya kidijitali – kuanzia kushiriki taarifa za kuokoa maisha hadi kupata fedha za kushughulikia hali ya dharura. Mkakati wa Muda Usio Mrefu wa UNEP unapendekeza kutumia zaidi teknolojia za kidijitali ili kuchochea matumizi na uzalishaji wa bidhaa kwa njia endelevu.



UNEP ina uhusiano na zaidi ya kampuni 17 za kiteknolojia ambazo ni pamoja na Microsoft, Google na LinkedIn. Kama mtunzaji wa vipimo 25 vya Malengo 6 ya Maendeleo Endelevu, UNEP imeunda mbinu za kukusanya data ili kupima maendeleo. UNEP pia ilifikia viwango vipya vya ubunifu, ikishirikiana na Google, NASA na mashirika mengine ili kuchunguza mifumo ya ekolojia, kwa kutumia senza, data ya setilaiti na teknolojia nyinginezo.

World Environment Situation Room hutoa habari kwa umma pamoja na data husus kuhusu maswala ya mazingira kwa Nchi Wanachama, Vikosi vya UN Nchini na Makubaliano ya Kimataifa ya Mazingira. Kuunga mkono mchakato wa UN wa Kuleta Mabadiliko, jukwaa hilo huwezesha nchi kuewelewa maswala ya mazingira, ambayo husababisha msingi wa Utathmini wa Kawaida wa Nchi, na kuwezesha nchi Zinazoshirikiana na UN katika Mipangilio ya Maendeleo Endelevu na zinazoripoti.

UNEP pia ilisonga mbele na badiliko lingine la kidijitali: kufanya mikutano kati ya serikali mitandaoni Makubaliano ya Carpathian, Makubaliano ya Vienna, Mkataba wa Montreal Makongamano ya Wanchama, na mikutano ya wawakilishi wa kudumu wa Kamati ya UNEP yote ilifanyika kwa mtandao kwa mara ya kwanza kabisa.



# Jinsia na Usawa



Kadiri ulimwengu unavyotambua ubaguzi wa rangi, ubaguzi wa jinsia na mapendeleo yaliyotokana na maandamano ya Black Lives Matter na #MeToo, UNEP imepitisha ujumbe kwamba sayansi inapaswa kuwa wazi kuhusu ubaguzi inayoendeleza na kuchukua hatua ya kurekebisha. UNEP imetaka kuwe na uwakilishi mkubwa wa wahamasishaji wa kimataifa na kuwa jinsia zote watu wa asili zote, dini zote na mataifa yote yashirikishwe.

UNEP inajitahidi kuongeza idadi ya wawakilishi. Usawa wa kijinsia unaboreka, huku asilimia 61 ya wafanyikazi wa UNEP ikijumuisha wanawake– ingawaje ukosefu wa usawa wa kijinsia kwa kuzingatia kanda bado ni changamoto inayopaswa kukabiliwa. Katika wafanyakazi wa ngazi ya juu, bado UNEP ina kazi ya kufanya, huku kukiwa na asilimia 43 ya wafanyikazi ambao ni wa kike. UNEP iliimarisha mbinu yake ya kupata usawa kupitia mfumo mpya wa Mazingira na Jamii Endelevu, ambayo inahakikisha mbinu inayozingatia haki ya binadamu kwa programu na miradi.

Nyingi ya kazi za UNEP katika mwaka wa 2020 zilijikita kwa haki na usawa kwa wote wanaohudumiwa na shirika hilo. Kwa mfano Ripoti ya Adaptation Gap inahusu kuhakikisha kwamba jamii zinazoweza kuathiriwa zinapata msaada wanaohitaji ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Katika miradi mingine, UNEP inahakikisha kuwa wanawake wanapata fursa sawa za ajira na kipato: kwa mfano huko Viet Nam, ambako mradi ambao bado unafanyiwa majaribio na wanawake wa UN unanufaisha biashara za wanawake zinazotumia nishati jadidifu. Mradi huo – ambao pia unaendeshwa huko Bangladesh na Cambodia – unalenga kuimarisha jitihada hizo ili kusaidia kuhusisha maswala ya kijinsia katika NDCs za nchi.

## Kutunza haki za mazingira na wahamasishaji

Ukiukaji wa haki za mazingira na za ardhi ya jamii – mara nyingi jamii za kiasili na wanawake – unaongezeka, huku mamia ya watu wakiuawa kila mwaka. UNEP ilifanya kazi na Ofisi ya UN ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu ili kuimarisha haki za mazingira na utekelezaji wake. Ushirikiano huo wa pamoja ulisaidia Nchi kuridhia Azimio la Usimamizi wa Haki ya Binadamu ya UN baada ya kutambua haki za mtoto kupitia mazingira salama. Ushirikiano huo pia unaonekana kupitia Azimio la Bunge la Ulaya, ikitaka mkakati wa EU ilinde haki ya mazingira salama.

Wakati uo huo, miaka ya kusaidiaa Phyllis Omido, mhamasishaji MKenya, ulimsaidia Omido na jamii yake kushinda kesi na kupata dola milioni 13 ya Marekani ikiwa ni malipo ya uharibifu kwa mazingira na afya yao kutokana na sumu ya risasi iliyotoka kwa kiwanda kilicho karibu.



# Kubadili UNEP kwa Wakati Ujao Imara Zaidi

Ustawishaji wa 2020 wa Mikakati mipya ya Muda Mfupi (MTS) 2022-2025 ulifuata hatua zilizojumuisha na zilizo wazi, kushauriana na Nchi Wanachama, Makubaliano ya Kimataifa ya Mazingira, sekta ya kibinafsi, vikundi vya kidini na wafanyakazi. Rasimu ya mwisho ya mikakati itawasilishwa kwa Nchi Wanachama katika UNEA-5 mwishoni mwa Februari 2021.

Mikakati na Programu ya Kazi (PoW) shirikishi zimekusudiwa kusaidia kuleta mabadiliko yafaayo ili kukabiliana na vyanzo vya mabadiliko ya tabianchi, mazingira na uharibifu wa bayoanuai, na kemikali na uchafuzi wa hewa. Mikakati hiyo inaenda sambamba na mifumo ya UNEP, utendakazi, utaratibu na desturi ili kuwa na athari kubwa zaidi.

Kipengee muhimu zaidi cha mabadiliko ya UNEP ni kufanya kazi vizuri na kwa njia bora zaidi katika muktadha wa mabadiliko ya UN. Kwa hivyo, Ofisi za UNEP za Ukanda zimeimarisha sana ushirikiano wao kupitia kwa Mabalozi wa Kudumu ili kuhakikisha kwamba vipengele vya mazingira vinajumuishwa vya kutosha katika kazi ya UN katika kiwango cha nchi.

Ulimwengu utakaposhinda COVID-19, kutakuwa na mengi ya kujifunza. Eneo moja ambalo UNEP inapangia kupatia kipao mbele ni kuhusisha wabia kupitia njia ya mtandao ili kuendeleza utendaji bora zaidi, kupunguza kuzalishaji wa gesi ya ukaa kuimarisha ushirikiano.



# Wito wa kuchukua hatua

Chanjo za COVID-19 zinapoendelea kuandaliwa, ulimwengu unaweza kuanza kuwa na matumaini kwamba janga hilo litaisha karibuni. Lakini hili haliwezi kumaanisha kurudia jinsi wengi wetu tulivyoishi awali. Ni lazima ulimwengu utumie mwaka ujao kufanyiza wakati ujao ulio mwangavu zaidi, salama zaidi kwa mazingira.

Sera zenye malengo makubwa na uwekezaji ulio salama kwa mazingira zinahitaji kutumiwa – ikujumuisha matumizi na uzalishaji endelevu. Ahadi zilizotolewa na Taifa zinapaswa kuimarishwa na kutangazwa kufikia mkutano ujao wa tabianchi huko Glasgow, UK, na ahadi hizi kubadilishwa na kuwa matendo. Mfumo wa bayoanuai ulio imara zaidi baada ya 2020 unahitaji kuamuliwa mwaka huu huko Kunming – na ahadi za kuchukua hatua katika ngazi zote na katika kila sekta. Kongamano la Kimataifa la Kusimamia Kemikali lazima liweke mikakati thabiti zaidi itakayotumika baada ya 2020 kuhusiana na kemikali na takataka. Na Muongo wa UN wa Koboresha Mifumo ya Ekolojia lazima ufaulu.

Mabadiliko makubwa hayatakuwa rahisi. Yanahitaji kila mmoja wetu, popote alipo,  kila siku, kuchukua hatua. Lakini ikiwa kuna jambo moja ambalo mwaka wa 2020 umetufundisha, ni kwamba jamii yote ya ulimwengu mzima inaweza kufanya mabadiliko makubwa haraka. Ulimwengu unapojitayarisha kuleta mabadiliko kama hayo kwa sayari, UNEP itakuwepo katika kufuatilia kila hatua, kutoa sayansi, ujuzi na msaada kwa watu na kwa sayari.



# Habari za Kweli za Kifedha




* Bajeti ya Kawaida inajumuisha UNDA

## Wachangiaji 15 wakuu wa Mfuko wa Mazingira katika mwaka wa 2020 kwa mamilioni ya dola za Marekani




## Wachangiaji 15 wakuu wa Mfuko wa Shughuli Hususa katika mwaka wa 2020 kwa mamilioni ya dola za Marekani




Chapisho hili linaweza kuchapishwa tena lote au sehemu yake katika njia yoyote ili kuelimisha au kwa kusudi la kutofanya biashara bila ruhusa maalum kutoka kwa wachapishaji halali ili mradi tu chanzo kitambulishwe. Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa litathamini kupokea nakala ya kitabu chochote ambacho kinatumia chapisho hili kama chanzo chake. Chapisho hili halipaswi kutengenezwa kwa kusudi la kuuzwa tena au makusudi mengine yoyote ya kibiashara kabla ya kupata ruhusa kutoka kwa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa. Kujumuishwa kwa mashirika ya maeneo ya kijiografia katika ripoti hii, na uwasilishaji wa habari hapa, hakurejelei maelezo ya mawazo yoyote kwa upande wa mchapishaji au mashirika yaliyohusika kuhusiana na hali ya kisheria ya nchi, eneo au mahali, au mamlaka yake, au kuhusiana na kuweka mipaka. **Kwa habari zaidi: unep.org/ripotiyakilamwaka**

©Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa, 2021